

Mzumbe, eGA kuboresha huduma kiteknolojia

Lilian Lucas, Mwananchi
llucas@mwananchi.co.tz

Morogoro. Chuo Kikuu Mzumbe kimesaini Mkataba wa Makubaliano ya ushirikiano wa huduma za kitaaluma na teknolojia na Mamila ya Serikali Mtandao Tanzania (eGA) kwa lengo la kuendelea kuboresha huduma za kitaaluma na teknolojia zinazotolewa na chuo hicho.

Akizungumza wakati wa kusaini makubaliano hayo jana njini hapa, Kaimu Makamu Mkuu wa Mzumbe, Profesa William Mweg-

oha alisema lengo ni kuimarisha mifumo ya kidijitali na kuongeza wataalamu katika kutoa huduma za kitaaluma ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kukuza ufanisi wa programu zinazotolewa na chuo.

Hivyo, alisema makubaliano hayo yatasaidia kubadilishana uzoefu na ujuzi kati ya Chuo Kikuu Mzumbe na eGA.

Awali, akizungumza katika hafla hiyo, Kaimu naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu wa Mzumbe, Dk Eliza Mwakasangula alisema makubaliano hayo ni matokeo

ya mkutano wa tatu wa Tehama uliofanyika Jijini Arusha kuanzia Februari 8 -12, 2023.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Uwezesaji katika Mamila ya Serikali Mtandao, CPA Salum Mussa, alikishukuru na kikipongeza chuo hicho kwa hatua ya kuboresha na kuimarisha ushirikiano na kuwa mionganini mwa taasisi za elimu ya juu zinazoshirikiana na eGA moja kwa moja.

Alisema eGA itaendelea kushirikiana ili kufikia malengo.



Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Profesa William Mwigoh (kulia) na Mwakilishi wa mkurugenzi mkuu wa Mamila ya Serikali Mtandao (eGA), Salum Rugambwa wakisaini.

Majaliwa ateta na wafanyakazi ubalozi Italia

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwanchipapers@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amekutana na kufanya mazungumzo na watumiishi wa ofisi ya Ubalozi wa Tanzania nchini Italia na kuwaagiza waendelee kuimarisha uhusiano wa kihistoria ulipo kati ya nchi hizo mbili.

Majaliwa alitoa maagizo hayo juu jioni, akiwa nchini humo, ambaopo alisema Tanzania inaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye sekta za kilimo, elimu, mifugo na afya, hivyo wao waendelee kufanya kazi kwa bidii, weledi na kutangaza fursa zilizopo nchini ili Taifa linufaikie na uwepo wao nchini Italia.

"Nchi ipo salama, uchumi unaendelea kukua na lugha yetu kwa sasa ni maendeleo ya nchi na Serikali inaendelea kuimarisha sekta mbalimbali, ikiwemo ya kilimo, ambayo inawauanuwaish-

ZAWADI

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Access Microfinance Tanzania, Julius Ruwaichi (kulia) akikabidhi cheti cha shukurani mmoja wa wateja ambaao warmekuwa wakifanya vizuri na benki hiyo, Zacky Al Ruqeish Zahoor. Ofisa mtendaji huyo alkabidhi vyeti hivyo katika hafia ya uzinduzi wa mwezi wa huduma kwa mteja ilyofanyika katika Tawi la Access Microfinance Bank Lumumba mwishoni wa wiki na kuhudhuriwa na baadhi ya wateja, uongozi na wafanyakazi mbalimbali wa benki hiyo. Na Mpigapicha Maalumu



UHUSIANO

Mbarawa: Tutaitumia TPA kujitanua

Mwandishi wetu, Mwananchi

Dar es Salaam. Wakati Mamila ya Bandari Tanzania (TPA) ikifungua ofisi zake nchini Zimbabwe, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa amesema wamejipanga kuyafikia masoko yaliyopo nchi jirani.

Waziri Mbarawa alisema Tanzania na Zimbabwe zimekubaliana kutafuta ufumbuzi wa kero zinazokwamisha kasi ya ukuaji wa biashara katika ushoroba wa Dar es Salaam, hasa ukitegemea bandari.

Akizungumza katika haffla ya ufunguzi wa ofisi za TPA uliofanyika siku chache zilizopita nchini Zimbabwe, Waziri Mbarawa alisema ufumbuzi huo ni pamoja utekelezaji wa miradi mipy ya upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam wa kujenga gati mbili (namba 12 hadi 15) na kutumia eneo lilioku-